HOTUBA YA NDUGU MOHAMMED KHAMIS ABDULLA, KATIBU MKUU, WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI, KATIKA HAFLA YA MAKABIDHIANO YA MASHINE SAIDIZI (PERSONAL DEVICE ASSISTANCE - PDA) KWA SHIRIKA LA POSTA TANZANIA KUTOKA MFUKO WA MAWASILIANO KWA WOTE JIJINI DODOMA, TAREHE 12 JULAI, 2024

1. Brigedia Jenerali (Mstaafu) Yohana Ochollo Mabongo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Posta Tanzania;
2. Bi. Salome Kessy, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
3. Bi. Justina Mashiba, Mtendaji Mkuu, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF);
4. Ndugu Maharage Ally Chande, Postamasta Mkuu, Shirika la Posta Tanzania;
5. Menejimenti na Watumishi wa Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.
6. Menejimenti na Watumishi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote pamoja na Shirika la Posta Tanzania;
7. Watumishi Wenzangu
8. Ndugu wanahabari;

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi MUNGU mwingi wa rehema kwa kutujalia sote afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya hafla ya makabidhiano ya mashine zaidizi kwa shirika la posta kutoka mfuko wa mawasiliano kwa wote.

Watumishi Wenzangu;

Naomba kutumia fursa hii kuishukuru Bodi na Menejimenti ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Shirika la Posta Tanzania (TPC) kwa ushirikiano mlioufanya katika kuhakikisha mnakuwa wabunifu na mnaendana na kasi ya ukuaji wa Teknolojia katika kurahisisha utoaji wa Huduma za Posta **Hongereni sana!**

Lakini pia, nimefarijika sana kuwa sehemu ya hafla hii na kushuhudia makabidhiano ya mashine hizi saidizi zinazojulikana kama "Personal Device Assistance" zilizonunuliwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na leo nitazikabidhi kwa Shirika la Posta Tanzania (TPC). **Hili ni jambo jema sana**

Watumishi Wenzangu;

Jitihada mnazozifanya zinalenga kurahisisha utoaji wa huduma kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano. Hii ni ishara tosha ya namna bora ya Utekelezaji wa Sera, Sheria na kanuni za Taasisi zenu katika kuhakikisha Huduma za Mawasiliano ya Posta zinaboreshwa, ili kuendana na mapinduzi yanayoendelea katika Sekta ya Posta ambayo yanachochewa na ukuaji wa matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma za Posta Pamoja na kukabiliana na ushindani uliopo katika Sekta na kuhakikisha kuwa Watanzania wengi wanapata fursa ya kuunganishwa na mifumo rasmi ya kuhudumia jamii kwa urahisi kwa lengo la kukuza uchumi wa wananchi na Taifa letu kwa ujumla.

Watumishi Wenzangu;

Shirika la Posta la Tanzania lina jukumu kubwa la kuiunganisha jamii yetu ndani na nje ya nchi kwa kupokea, kusafirisha na kufikisha nyaraka, barua, vipeto na vifurushi. Huduma hizi zimekuwa bora kutokana na matumizi ya teknolojia, hivyo kitendo cha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) kulipatia Shirika la Posta Tanzania vitendea kazi hivi maarufu kama PDA, kutaimarisha uwezo wa Shirika kutoa huduma za usafirishaji kwa ufanisi na uhakika kote nchini. Vifaa hivi vitawezesha ufuatiliaji wa vifurushi na

vipeto vya wateja kwa wakati, usimamizi bora, uhifadhi wa taarifa za wateja, na kuimarisha mawasiliano na wateja hivyo kuboresha uendeshaji wa shughuli za posta kuendana na mahitaji ya sasa ya soko yanayohitaji matumizi ya teknolojia.

Watumishi Wenzangu;

Uwepo wa Mashine hizi ndani ya Shirika la Umma, kutaendana na maono ya Serikali ya Awamu ya Sita yanayolenga **kujenga uchumi wa kidijitali** unaoenda sambamba na kasi ya maendeleo ya teknolojia duniani. Kupitia vifaa hivi vinavyotolewa leo na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, vitawezesha Shirika kuwafikia watanzania wengi zaidi na kuhakikisha hata maeneo ya mbali yanafaidika na nguvu ya teknolojia, lakini pia kuzalisha fursa za kiuchumi na maendeleo.

Watumishi Wenzangu;

Kama alivyoeleza Postamasta Mkuu, uwepo wa mashine hizi ndani ya Shirika la Posta Tanzania kutaimarisha shughuli za usafirishaji wa vifurushi vya wateja kwani zitatumika kuingiza taarifa sahihi za wateja, ufuatiliaji wa nyaraka na vifurushi vya wateja hivyo kuondoa upotevu wa taarifa za wateja hasa zile zinazoandikwa kwenye karatasi. Wafanyakazi watatoa

taarifa sahihi na kwa haraka kwa wateja wakati wa upokeaji na ufikishwaji wa vifurushi, hivyo kulifanya Shirika kuendelea kuaminika zaidi kwa wateja na Watanzania kwa ujumla.

Watumishi Wenzangu;

Kwa kuwa mashine hizi zinabebeka (portable) ukilinganisha na kompyuta za mezani, zina uwezo wa kutumika kama njia ya mawasiliano kati ya wafanyakazi na wateja mahali popote walipo hivyo kurahisisha namna ya kushughulikia maulizo na malalamiko ya wateja. Kwa lugha rahisi ninaweza kusema mashine hizi, zitaboresha uwezo wa uendeshaji na utoaji wa huduma zinazokidhi matarajio ya wateja na vigezo vya ubora wa huduma Kitaifa na Kimataifa.

Watumishi Wenzangu;

Wizara itaendelea kuweka na kuboresha miongozo ya Kisera na Kisheria katika kuhakikisha jitihada mnazozifanya zinakuwa na tija na zinagusa maisha ya watanzania. Ni matarajio yetu kwamba tutaliona Shirika la Posta Tanzania likiendelea kuwa bunifu likitoa huduma zake kwa njia za kisasa za kidijitali na zaidi kuwafikia wateja wengi ndani na nje ya nchi. Nafurahi kuona mageuzi ya kidijitali yanayofanywa ndani ya Shirika hili

ambayo yana chachu katika kuchangia ukuaji wa uchumi. Muendelee kutumia fursa za teknolojia zinazoibukia kwa lengo la kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja wenu.

Watumishi Wenzangu;

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kama ulivyo wajibu wake, umekuwa kichocheo muhimu cha maendeleo ya mawasiliano kwa wote nchini kupitia jitihada mbalimbali zinazofanywa. Hivyo nitumie fursa hii tena kuipongeza Bodi na Menejimenti ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa jitihada mbalimbali ambazo mmeendelea kuzifanya katika kuhakikisha huduma za Mawasiliano zinapatikana kwa ubora, gharama nafuu na kufika maeneo yote nchini yasiyo na mvuto wa kibiashara pamoja na maeneo yote ya kimkakati.

Watumishi Wenzangu

Kwa mara nyingine tena niwashukuru na kuwapongeza sana Watendaji Wakuu wa taasisi hizi za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Shirika la Posta Tanzania (TPC) kwa maono haya yenye kusaidiana katika kuleta mabadiliko ya utendaji kazi ndani ya Taasisi zenu na kuwanufaisha Watanzania Wote.

Watumishi Wenzangu

Baada ya maneno haya, sasa nipo tayari kushuhudia utiaji Saini Hati ya makabidhiano kati ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Shirika la Posta Tanzania (TPC) pamoja na kukabidhi Vifaa Saidizi (PDA) kama ilivyopangwa.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Asanteni sana kwa kunisikiliza.